# Mashariki ya Kati: Ukame Kuwageuza Watu kuwa Wahamiaji wa Milele, Waliomo katika Hatari ya Kuvutiwa na Ugaidi?

Imeandikwa na Baher Kamal

*Makala hii ni sehemu ya makala maalum ya IPS ya Kuadhimisha Siku ya Dunia ya Kupambana na Maafa ya Jangwa na Ukame, yaliyofanyika Juni 17.*



*Kwa hisani ya: UNCCD*

ROME, Juni 13, 2017 (IPS) - Ulimwenguni kote, uharibifu wa ardhi, ukame mkali na upungufu wa mazao unaotokana na ongezo la ardhi kuwa jangwa ni changamoto ambazo zitalazimu idadi kubwa ya watu kuhama makwao na kuhamia maeneo mengine. Katika eneo mahususi la Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Afrika (MENA), hali kama hiyo inamaanisha kwamba kuna hatari ya kuwafanya watu kuvutiwa zaidi na ugaidi au hata makundi ya ugaidi.

Hitimisho hili linatokana na hali ilivyo katika eneo la MENA, eneo ambalo ni makao kwa watu wasiopungua milioni 400. Eneo hili ni mojawapo ya maeneo yaliyoathiriwa sana na ukame na kuenea kwa hali ya jangwa kwa haraka.

Hali ni kwamba wanasayansi kadhaa wanaotumia mbinu za kisayansi wamekuwa wakishughulikia hali ya kutisha ambayo eneo la MENA linaweza kubadilika kuwa katika miongo michache ijayo kuanzia sasa, kasi ya haraka zaidi itakuwa kufikia mwaka wa 2040.

Mambo mengi yameonekana kutokana na utafiti huu – ambao ulitoa ripoti zilizoeleza wazi wazi hali hii. Angalia, kwa mfano, makala ya Ushahidi Mpya Unathibitisha Hatari Kwamba Watu Hawataweza Kuishi katika Eneo la Mashariki ya Kati: New Evidence Confirms Risk That Mideast May Become Uninhabitable. Na makala ya; Je, "Watu Hawataweza Kuishi" katika Eneo la Mashariki ya Kati (Will the Middle East Become 'Uninhabitable'?)

Jumuiya ya kimataifa itaadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Hali ya Jangwa Duniani (WDCD) tarehe Juni 17, na mada ya siku hiyo itakuwa: "Ardhi Yetu. Makao Yetu. Maisha Yetu." Siku hiyo itachunguza uhusiano muhimu uliopo kati ya uharibifu wa ardhi na uhamiaji wa watu kuelekea maeneo mengine.

WDCD huadhimishwa kila mwaka ili kukuza uelewa wa umma kuhusu jitihada za kimataifa za kupambana na hali ya jangwa duniani.

**Je, Hali ya Jangwa Inahusu Nini?**

Jangwa ni uharibifu wa ardhi katika maeneo yenye ukame, maeneo yaliyoainishwa kuwa hayapokei mvua ya kutosha na maeneo yenye hali za joto kali, zinazochangia eneo kukauka. Kulingana na Umoja wa Mataifa, hali ya jangwa inasababishwa hasa na shughuli za binadamu na tofauti za hali ya hewa.

“Hali ya kuwepo kwa jangwa hakumaanishi kwamba kuna upanuzi wa maeneo ya majangwa yaliyopo. Inatokea kwa sababu mazingira ya maeneo yaliyokauka ambayo hufikia hadi asilimia 33 ya sehemu yote ya ardhi duniani yamo katika hatari kubwa ya kutumiwa vibaya na kuna matumizi mabaya ya ardhi. Umasikini, kutokuwa na utulivu wa kisiasa, ukataji miti, kutumia zaidi ardhi kwa ajili ya malisho ya wanyama na mbinu mbovu za kunyunyuzia mimea maji zinaweza kudhoofisha uzalishaji wa ardhi.”

Umoja wa Mataifa unaeleza kwamba, zaidi ya watu milioni 250 wanaathirika moja kwa moja kutokana na kuwepo kwa hali ya jangwa, na karibu watu bilioni moja katika zaidi ya nchi mia moja wamo hatarini."Watu hawa ni pamoja na wananchi wengi ambao ni maskini zaidi, waliotengwa zaidi na wasiojiweza kisiasa.”



*Bandiagara, mji mdogo katika sehemu kame ya kati nchini Mali ambako wakulima wa Dogoni wanakoishi. Picha ni kwa hisani ya: UN Photo/Alejandra Carvajal*

Kulingana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Hali ya Jangwa (UNCCD), Siku ya Dunia ya Kupambana na Hali ya Jangwa ni siku ya kipekee ya kumkumbusha kila mtu kwamba urekebishaji wa uharibifu wa ardhi (land degradation neutrality -LDN) unaweza kufanikiwa kupitia utatuzi wa matatizo ya kijamii, jamii kuhusika kwa uthabiti na ushirikiano katika ngazi zote.

“Uharibifu wa mazingira, ukosefu wa utulivu wa kisiasa, ukosefu wa usalama wa chakula na umaskini ndizo sababu kuu zinazosababisha changamoto za uhamiaji na maendeleo.”

Kwa kweli, sekretarieti ya UNCCD iliyoko mjini Bonn- inawakumbusha watu kwamba katika miaka 15 tu, idadi ya wahamiaji wa kimataifa ulimwenguni kote imeongezeka kutoka milioni 173 mwaka

wa 2000 hadi milioni 244 mwaka wa 2015.

**Ukame, Suala Kubwa Lisilojulikana**

Sekritarieti ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa inasema kwamba ukame ni suala tatanishi na linalonyemelea mazingira asili na kuleta athari kubwa zinazoathiri mifumo ya kijamii na kiuchumi na kuleta madhara makubwa kwa mazingira. Ukame unajulikana kusababisha vifo vingi na kusababisha watu zaidi kuhamia maeneo mengine kuliko msiba wowote wa asili.

Kufikia mwaka wa 2025, watu bilioni 1.8 watakuwa na uhaba mkubwa wa maji, na theluthi mbili za watu ulimwenguni watakuwa wanaishi katika hali ngumu za kupata maji.

UNCCD inaripoti kwamba mahitaji ya maji yanatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 50 kufikia mwaka wa 2050. Ongezeko la idadi ya watu linavyoendelea kukua, hasa katika maeneo ya ukame, watu zaidi na zaidi wanategemea vyanzo vya utoaji wa maji safi vilivyo ardhini ambayo vinaendelea kuharibiwa. Uhaba wa maji ni mojawapo ya changamoto kubwa zaidi ya karne ya ishirini na moja.

“Ukame na upungufu wa maji huzingatiwa kuwa maafa makubwa zaidi kati ya maafa yote ya asili, husababisha hasara za muda mfupi na za muda mrefu za kiuchumi na kimazingira pamoja na athari kubwa kwa sekta zingine." mkataba unaeleza.”

**Ukosefu wa Maji kwa Kiwango Kikubwa**

Umoja wa Mataifa hivi karibuni ulionya kuwa upatikanaji wa kila mwezi wa maji safi katika kanda la MENA kwa sasa unapungua kwa mara 10 kuliko kiwango cha wastani cha dunia. Aidha, joto la juu linaweza kufupisha majira ya kukuza mimea katika eneo la MENA kwa siku 18 na kupunguza mavuno ya kilimo kwa zaidi ya asilimia 27 kufikia asilimia 55 kufikia mwisho wa karne hii, asilimia hii iko chini sana.

Kulingana na shirika la Umoja wa Mataifa linaloongoza katika uwanja wa chakula na kilimo, hali inayofanya suala la ukosefu wa maji kuwa gumu zaidi ni kwamba rasilimali za maji safi katka eneo la MENA ni miongoni mwa chache zaidi duniani. Zaidi ya haya, rasilimali hizi zinatarajiwa kupungua kwa asilimia 50 kufikia mwaka wa 2050.

Aidha, asilimia 90 ya ardhi yote katika eneo hilo iko kati ya maeneo yenye ukame, nusu ukame na maeneo yaliyokauka, huku asilimia 45 ya jumla ya eneo la kilimo inakumbwa na hali ya ongezeko la chumvi ardhini, kupunguka kwa virutubishi ardhini na mmonyoko wa udongo unaosababishwa na upepo na maji, Shirika la Chakula na Kilimo Duniani la Umoja wa Mataifa (FAO) linaongeza kuelekezea hali ya MENA.

Ili kushughulikia suala hili, UNCCD inasema kuwa ili kupunguza athari hizi, maandalizi ya kukumbana na ukame ambayo yanakidhi mahitaji ya binadamu huku yakidumisha ubora wa kimazingira na mifumo asili yawepo. Maandalizi haya yanahitaji kujumuisha wadau wote ikiwa ni pamoja na watumiaji wa maji na watoa huduma za maji ili kufikia suluhisho la kushughulikia ukame.

"Hatua ya kupunguza madhara ya ukame inapaswa kutekelezwa kwa kuzingatia mifumo jumuishi ya mapema ya kuonya kuhusu ukame na kufuatilia mifumo hiyo, tathmini ya uwezo wa kuathirika na hatari ifanywe, matumizi ya mikondo ya maji, uhusiano kati ya matumizi ya maji na ardhi na mikakati mbalimbali ya kuwezesha watu kujikimu maishani hasa watu wanaoishi katika maeneo ambayo huathiriwa na ukame kuwekwa n.k. Kwa mfano, kukabiliana na uharibifu wa ardhi katika sehemu ya juu ya vyanzo vya maji huboresha uwezo wa kupata maji kwenye sehemu ya chini ya vyanzo hivyo vya maji.

Afya ya ardhi ni muhimu katika kutafuta suluhisho endelevu za kushughulikia utoaji wa rasilimali za maji na usimamizi wa rasilimali hizo za maji, Sekretarieti ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa inaelezea. "Ni muhimu kwa nchi kuchukua hatua kwa kutenda (badala ya kusema tu); kushirikiana katika ngazi ya kikanda (mbali na hatua zinazofanya katika kiwango cha nchi); kuchukua hatua zinazojumuisha sekta zote kikamilifu (badala ya kuzipa sekta mbalimbali majukumu tofauti tofauti) na kushughulikia ukame kama "hatari ya mara kwa mara" (badala ya 'mkasa') ni miongoni mwa suluhisho za kukabiliana na hali ya ukame."

Maadhimisho ya kimataifa ya # 2017WDCD yatafanyika tarehe 15 Juni, mjini Ouagadougou, Burkina Faso. Maadhimisho ya siku hiyo yatahudhuriwa na Waziri wa Mazingira na Mabadiliko ya Hali ya Hewa (le Ministère de l'Environnement, de l'Economie Verte et du Changement Climatique).

**Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Hali ya Jangwa Duniani (UNCCD)**

Mkataba huu ulianzishwa mwaka wa 1994. UNCCD ndio mkataba wa kipekee ambao umewekwa kisheria ili kushughulikia uhusiano kati ya mazingira na maendeleo ya matumizi ya ardhi kwa njia endelevu. Mkataba huu unashughulikia hasa maeneo yenye ukame, maeneo yanayopokea mvua kidogo na maeneo yaliyokauka ambayo hujulikana kama maeneo kame, ambapo baadhi ya mifumo ya mazingira na watu wanaopatikana katika eneo hilo wamo katika hatari ya kuathiriwa zaidi.

Nchi wanachama 195 zinafanya kazi pamoja ili kuboresha hali ya maisha ya watu katika maeneo kavu, kudumisha na kurejesha uzalishaji wa ardhi na udongo na kupunguza madhara ya ukame.

UNCCD imejitolea kuchukua mtazamo wa kushirikisha watu kuanzia kiwango cha chini kuelekea viwango vya juu. Mtazamo ambao unaleta hali ya kuwashirikisha watu wa eneo katika kukabiliana na hali ya jangwa na uharibifu wa ardhi. Sekretarieti inawezesha ushirikiano kati ya nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea, hususan katika maeneo ya uhamishaji wa maarifa na teknolojia kwa ajili ya usimamizi na matumizi endelevu ya ardhi.

Tofauti na jinsi suala la ardhi lilivyopana, kuna uhusiano wa karibu sana kati ya hali ya hewa na mifumo asili ya mazingira. UNCCD inashirikiana kwa karibu na Mikataba miwili ya Rio; (Mkataba wa Mifumo Asili ya Kimazingira) Convention on Biological Diversity (CBD) na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kushughulikia Mabadiliko ya Hali ya Hewa United Nations Framework Convention on Climate Change (UNFCCC), ili kukabiliana na changamoto hizi ngumu kwa kuchukua mtazamo unajumuisha nchi mbalimbali na kuleta nchi na wadau pamoja ili kushughulikia changamoto hizi kwa pamoja na kutoa njia bora za matumizi ya maliasili.